# HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI

File

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 05-06/05/2017

**KUMB. NA.32/2016/2017 – WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Diwani Mathei B. Makwinya | - | Kata ya Nyangao | -Mwenyekiti |
| 2. | Diwani Kassimu A.Namwete | - | Kata ya Kilangala | -Makamu Mwenyeki |
| 3. | Mhe. Hamidu Bobali (MB) | - | Jimbo la Mchinga | -Mjumbe |
| 4. | Diwani Ismail A.Ladda | - | Kata ya Nahukahuka | -Mjumbe |
| 5. | Diwani Abdul H.Njenga | - | Kata ya Longa | -Mjumbe |
| 6. | Diwani Omari R.Mpoyamboya | - | Kata ya Milola | -Mjumbe |
| 7. | Diwani Hassani O.Kunyong'onyea | - | Kata ya Mtama | -Mjumbe |
| 8. | Diwani Shafii F.Chilumba | - | Kata ya Mandwanga | -Mjumbe |
| 9. | Diwani Ally A.Njale | - | Kata ya Sudi | -Mjumbe |
| 10. | Diwani Manzi S.Selemani | - | Kata ya Chiponda | -Mjumbe |
| 11. | Diwani Halima R.Mwambe | - | Kata ya Mnara | -Mjumbe |
| 12. | Diwani Somoe H.Madodo | - | Viti maalum Mchinga | -Mjumbe |
| 13. | Diwani Sina J.Nyanga | - | Viti maalum Nangaru | -Mjumbe |
| 14. | Diwani Mkopi M.Mkopi | - | Kata ya Nyengedi | -Mjumbe |
| 15. | Diwani Hatibu O.Kambwili | - | Kata ya Nangaru | -Mjumbe |
| 16. | Diwani Saidi A.Naomari | - | Kata ya Mipingo | -Mjumbe |
| 17. | Diwani Victor D.Matanje | - | Kata ya Rutamba | -Mjumbe |
| 18. | Diwani Rashid H.Mkuya | - | Kata ya Navanga | -Mjumbe |
| 19. | Diwani Ismail A.Jolova | - | Kata ya Mtua | -Mjumbe |
| 20. | Diwani Ally Nampanda | - | Kata ya Nyangamara | -Mjumbe |
| 21. | Diwani Omari M.Liveta | - | Kata ya Mnolela | -Mjumbe |
| 22. | Diwani Bakari H.Ding'unde | - | Kata ya Pangatena | -Mjumbe |
| 23. | Diwani Ahmadi M.Mbonde | - | Kata ya Mtumbya | -Mjumbe |
| 24. | Diwani Mohamedi H.Chilumba | - | Kata ya Kiwalala | -Mjumbe |
| 25. | Diwani Karimu Nyanga | - | Kata ya Kilolambwani | -Mjumbe |
| 26. | Diwani Ally H. Mbilla | - | Kata ya Namupa | -Mjumbe |
| 27. | Diwani Mariamu Khalifa Abdallah | - | Viti maalum Mtama | -Mjumbe |
| 28. | Diwani Jumu A.Ndondi | - | Viti maalum Mchinga | -Mjumbe |
| 29. | Diwani Asha M.Mpalanga | - | Viti maalum Mipingo | -Mjumbe |
| 30. | Diwani Habiba H.Ngalama | - | Viti maalum Mnara | -Mjumbe |
| 31. | Diwani Fatuma I. Malindi | - | Viti maalum Nyangamara | -Mjumbe |
| 32. | Diwani Surdi S. Kanduru | - | Kata ya Namangale | -Mjumbe |
| 33. | Diwani Idarous Y.Manzi | - | Kata ya Mvuleni | -Mjumbe |
| 34. | Diwani Rajabu H.Mfaume | - | Kata ya Majengo | -Mjumbe |
| 35. | Diwani Rashidi Ninje | - | Kata ya Nachunyu | -Mjumbe |
| 36. | Diwani Hamisi M.Ngumbe | - | Kata ya Mchinga | -Mjumbe |
| 37. | Diwani Hamza H.Msagula | - | Kata ya Kitomanga | -Mjumbe |
| 38. | Diwani Mohamedi S.Mkulyuta | - | Kata ya Kiwawa | -Mjumbe |
| 39. | Diwani Bakari M.Nampoka | - | Kata ya Matimba | -Mjumbe |
| 40. | Diwani Costansia John Lupapa | - | Viti maalum Milola | -Mjumbe |
| 41. | Diwani Moza Todi Liganga | - | Viti maalum Mingoyo | -Mjumbe |
| 42. | Diwani Bi.Raya Mkwacha | - | Viti maalum Sudi | -Mjumbe |
| 43. | Diwani Hawa A. Mponda | - | Viti maalum Mingoyo | -Mjumbe |

**KUMB. NA. 32.1/2016/2017 – WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Nape Nnauye (MB) | - | Jimbo la Mtama<br>Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo. |

**KUMB. NA. 32.2/2016/2017 – WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Nd. Samwel W.Gunzar | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) – Katibu |
| 2. | Nd. Thomas Safari | - | Katibu Tawala Wilaya |
| 3. | Nd. Salum Mpili | - | Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 4. | Nd. Rashid Tullah | - | Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 5. | Nd. Iddi Mboweto | - | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 6. | Nd. Gervas Ngomano | - | Mweka Hazina (W) |
| 7. | Mwl.Alphonce Ngongi | - | Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 8. | Dkt. David E. Kwavi | - | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 9. | Nd. Wenceslaus Mbilango | - | Mratibu TASAF III |
| 10. | Nd. Mnyangara M.Kaguta | - | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 11. | Nd. Cosmas Mwantisya | - | Kaimu Afisa M/Jamii (W) |
| 12. | Nd. Haroni I. Kihara | - | Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 13. | Nd. Daniel Kasembe | - | Kaimu Afisa Ugavi (W) |
| 14. | Nd. Yolenda Makumbuli | - | Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI |
| 15. | Nd. Hamis Abdallah | - | Kaimu Afisa Uchaguzi |
| 16. | Nd. Aswile M.Mwasaga | - | Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) |
| 17. | Nd. Charles Mwaipopo | - | Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 18. | Nd. Rashidi Makujunga | - | Kaimu Afisa Biashara (W) |
| 19. | Nd. Bakari C. Omari | - | Katibu TSC (W) |
| 20. | Nd. Ramadhani Malele | - | Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Shule (W) |
| 21. | Nd. Leo Shabani | - | Afisa Ushirika |
| 22. | Nd.Majdi Mbale | - | Afisa TEHAMA |
| 23. | Nd. Nyamande Kazimiri | - | Mwanasheria wa Halmashauri |
| 24. | Nd. Dickson R.Kananda | - | Kaimu Afisa Usafirishaji |
| 25. | Nd. Msafiri Makonyole | - | Kaimu Afisa Ardhi (W) |
| 26. | Nd. Mbaraka M.Kilangai | - | Mhandisi wa Maji (W) |
| 27. | Dkt. Mbikilwa A. Zuberi | - | Kaimu Mganga Mkuu |
| 28. | Nd. Langula Madirisha | - | Katibu wa Afya |
| 29. | Nd.Charles Makama | - | Afisa Mazingira |
| 30. | Nd. Fadhili Livigha | - | Mwandishi wa vikao |

**KUMB. NA. 32.3/2016/2017 – WAALIKWA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Nd. Shaibu Ndemanga | - | Mkuu wa Wilaya – Lindi. |
| 2. | SP Augustino G.Titus | - | OCD |
| 3. | Nd.Joseph J.Ngonyani | - | Kutoka Jeshi la Zimamoto (W)-Lindi |
| 4. | Nd. Fidea Peter | - | Kutoka Takukuru |

**KUMB. NA. 32.4/2016/2017- WAKARIBISHWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Nd. Bahati Samweli | - | Mwandishi wa RAF |
| 2. | Nd. Mwanja Ibadi | - | Mwandishi wa gazeti la Mwananchi |
| 3. | Nd. Keneth Kisura | - | Mwandishi wa gazeti la Habari Leo |
| 4. | Nd.John Sembe | - | Mwandishi wa Azam Media |

**KUMB. NA. 33/2016/2017 – KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao Katibu alimjulisha Mwenyekiti kuwa akidi ya wajumbe imetimia hivyo, alimkaribisha kufungua na kuendesha kikao. Mwenyekiti aliwaomba wajumbe wawe watulivu kujadili

dondoo zilizowasilishwa, alisisitiza suala la mshikamano kati ya Waheshimiwa Madiwani na Wataalam. Alifungua kikao saa 4.00 asubuhi.

**KUMB. NA. 34/2016/2017 – KUTHIBITISHA AGENDA.**

Dondoo za agenda za kikao cha Baraza la Madiwani zilizowasilishwa na kuthibitishwa ni zifuatazo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kupokea na kujadili taarifa kutoka kwenye Kata
4. Maswali ya papo kwa papo
5. Kusoma na kuthibitisha mihtasari ya vikao vya tarehe 31/01 – 01/02/2017 na 21/22/01/2017 (kikao maalum).
6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya tatu mwezi Januari – Machi,2017-04-25
7. Taarifa ya mihtasari ya vikao vya Kamati za kudumu
    (i) Kamati ya fedha, Utawala na Mipango
    (ii) Kamati ya Elimu Afya na maji
    (iii) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    (iv) Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
8. Mapendekezo ya marekebisho ya kanuni za kudumu za uendeshaji mikutano.
9. Maelekezo ya utoaji na usimamizi wa mikataba na zabuni kwa Serikali za Mitaa
10. Kufunga kikao

**KUMB. NA. 35/2016/2017 – KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA KUTOKA KWENYE KATA.**

Wajumbe walipata nafasi ya kuwasilisha taarifa kutoka kwenye Kata zao. Taarifa hizo ziliwasilishwa kwa kuzingatia kanuni ya 25 ya uendeshaji wa vikao vya Halmashauri. Hivyo zilihusisha mambo yafuatayo:-

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Kata zao ambapo ilihusisha ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, masuala ya elimu, shughuli za kilimo na ufugaji. Taarifa zilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano.

Katika kujadili taarifa hizo kuhusu suala la kilimo wajumbe walikumbusha kwamba Kata ya Kilolambwani na Mvuleni bado zinasumbuliwa na wanyama waharibifu hasa Tembo ambao wanaharibu mazao ya wakulima. Kwa hali hiyo,

**ILISHAURIWA kuwa**, kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira iendelee kufuatilia ili eneo hilo lijengwe kituo kidogo cha kudhibiti wanyama waharibifu.

Pia, wajumbe walieleza tatizo la mnyauko wa mazao ya mahindi katika Kata ya Navanga. Katika kujibu hoja hizo Mkurugenzi Mtendaji (W) kuhusu tatizo la wanyama waharibifu alieleza kuwa ushauri uliotolewa wa kujenga kituo kidogo umezingatiwa, utekelezaji halisi utawasilishwa kupitia kwenye kikao cha Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.

Kuhusu mazao yaliyonyauka, Idara ya kilimo itafuatilia hata hivyo, alisisitiza kuwa taarifa za aina hiyo ziwe zinawasilishwa haraka sio lazima kungoja wakati wa kikao.

Aidha, wajumbe walikumbusha na kusisitiza kwamba Kata zote ambazo zinatekeleza miradi yake kwa njia ya wananchi kujitolea kazi zilizondani ya uwezo wao Halmashauri ielekeze nguvu zake kwa kuwaunga mkono kwa kuwapelekea vifaa ambavyo vipo nje ya uwezo wao kwa mfano, Kata ya Matimba kuna miradi mipya ya ujenzi wa darasa na nyumba ya mwalimu katika shule ya msingi.

Kutokana na maelezo ya wajumbe Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa miradi hiyo itatembelewa na kuonwa ili kuelewa imefikia hatua gani za ujenzi.

Pia, wajumbe walikumbusha kuwa baadhi ya Kata bado zina matatizo ya maji kwa mfano, Kata ya Longa katika kijiji cha Narwadi hasa kipindi cha kiangazi kwa hiyo,
**ILISHAURIWA kuwa**, kamati ya Elimu, Afya na Maji iendelee kufuatilia ili kubainisha maeneo mengine yenye matatizo ya maji.

Katika kujibu hoja hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji alieleza kuwa suala hilo Kamati yake itafuatilia na itabainisha miradi mbalimbali.

Aidha, kwa upande wa shughuli za Afya hasa suala la watumishi kwenye zahanati wajumbe walieleza kuwa, kutokana na zoezi la uhakiki vyeti ambalo limesabibisha kuondolewa kwa baadhi ya watumishi kwa sababu ya kukosa vyeti halali vya kidato cha nne, kuna Zahanati zimekosa watumishi kwa mfano, Zahanati ya Sudi na Mkanga II. Kwa hali hiyo

**ILISHAURIWA** kuwa, suala hilo lishughulikiwe na Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ili pengo hilo lizibwe na wananchi wapate huduma.

Pia wajumbe walisisitiza kwamba ofisi iandae mikakati itakayowezesha Zahanati zilizojengwa na kukamilika zianze kutumika na wananchi wapate huduma.

Kuhusu taarifa ya Kata ya Rutamba kwamba kuna kituo cha kuuza madawa ya kulevya na kwamba jeshi la polisi ngazi ya Wilaya lilifanya msako mara mbili lakini wanaouza hawajakamatwa kutokana na maelezo hayo ilishauriwa kuwa wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi.

Aidha, wajumbe walishauri kuwa miundombinu ya Kituo cha Afya Mtua Longa iboreshwe kwani ni chakavu. Katika kujibu hoja hiyo Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa suala hilo likumbushwe wakati wa bajeti.

Pia, wajumbe walisisitiza na kushauri kuwa shule za msingi na sekondari zenye upungufu mkubwa wa madarasa wakati wa bajeti zipewe kipaumbele kwa mfano, shule ya Msingi Mmongomongo iliyopo kata ya Navanga. Ilisisitizwa kuwa, wakati wa bajeti kamati ya Elimu, Afya na Maji ikumbuke ili suala hilo liwekewe kipaumbele.

Aidha, katika taarifa ya Kata ya Matimba ilielezwa na kukumbushwa kuwa bado kuna tatizo la miundombinu ya barabara ya Chikonji – Nangaru. Kutokana na tatizo hilo,
**ILISHAURIWA kuwa**, maeneo yote korofi yafanyiwe marekebisho, Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ifuatilie suala hilo.

Kuhusu, shughuli za kiutawala wajumbe walikumbushwa kwamba changamoto kubwa katika maeneo yao ni upungufu wa watumishi hasa Watendaji wa vijiji walioajiriwa na Maafisa Ugani hivyo. Katika kujibu hoja ya watumishi Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa Ofisi inafuatilia suala hilo Idara kuu ya Utumishi ili itolewe kibali cha kuajiri.

Baada ya majadiliano ya kutosha kuhusu taarifa kutoka kwenye Kata wajumbe kwa ujumla, **WALISHAURI** kuwa, taarifa zilizowasilishwa kutoka kwenye Kata Mkurugenzi Mtendaji (W) azifanyie uchambuzi ili changamoto mbalimbali zilizotolewa na wajumbe zibainishwe na ziwasilishwe kwenye vikao husika vya Kamati za kudumu kwa ajili ya kwenda kujadiliwa.

**KUMB. NA. 36/2016/2017 – MASWALI YA PAPO KWA HAPO**
Maswali ya papo kwa hapo yaliwasilishwa kwenye kikao. Maswali hayo yaliulizwa kwa mujibu wa kanuni za kudumu za mikutano Na.23.

Wajumbe waliopata nafasi ya kuuliza maswali walikuwa wafuatao:-

| Na | Swali | Jibu |
|---|---|---|
| 1 | **Mjumbe Victor Matanje.** Alipenda apewe maelezo iwapo wataalam wanatoa siri za vikao watawajibishwa, na je akibainika ametoa siri utaratibu gani utachukuliwa. | Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu kuwa sheria za kiutumishi zipo na kila mtumishi amekula kiapo cha kutunza siri, hivyo akibainika atachukulia hatua za kinidhamu. |
| 2 | Mjumbe **Karimu Nyanga.** Alitaka kujua kwa vile Halmashauri ina wageni wengi kuna mkakati gani wa kudhibiti Ardhi isitolewe kiholela.<br><br>Pia, **mjumbe Karimu Nyanga** alipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Alipenda apewe maelezo ni lini mzungu aliopo eneo la Mchinga taarifa zake zitapatikana za kuthibitisha kwamba ni mwekezaji. | Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu kuwa utaratibu wa kupata ardhi upo kwa kuzingatia sheria zilizopangwa hivyo, sheria itazingatiwa wakati wa kutoa Ardhi.<br><br>Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu kuwa suala hilo atalifuatilia na taarifa zitawasilishwa kwenye Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira. |

**KUMB. NA. 37/2016/2017- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA VIKAO VYA TAREHE 31/01 – 01/02/2017 NA 21/22/01/2017 (KIKAO MAALUM).**

Mihtasari ya vikao vya Baraza la Madiwani tarehe 31/01 – 01/02/2017 na 21-22/01/2017 (Kikao maalum) iliwasilishwa. Baada ya wajumbe kusoma waliridhika na kuridhia isainiwe. Kwa hali hiyo,

***ILIAZIMIWA*** kuwa, Mihtasari ya Mkutano wa Baraza la Madiwani, vikao vya tarehe 31/01 – 01/02/2017 na 21-22/01/2017 (Kikao maalum), ilikubaliwa na kusainiwa.

**KUMB. NA. 38/2016/2017 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU MWEZI JANUARI – MACHI MWAKA 2017**

Taarifa ya Utekelezaji Miradi ya Maendeleo Robo ya tatu mwezi Januari – Machi,2017 iliwasilishwa. Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri iliidhinishiwa kutumia Tshs.14,783,334,908/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aidha, kati ya fedha hizo Tshs.12,512,991,865/= ni fedha zilizoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 na Tshs.2,270,343,043/= ni fedha zilizosalia katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Lifuatalo ni Jedwali linaloonyesha Muhtasari wa Mapato na Matumizi ya Fedha za Miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Machi,2017.

| NA | CHANZO CHA FEDHA | BAJETI IDHINISHWA TSHS. | FEDHA POKELEWA TSHS. | FEDHA TUMIKA TSHS. | BAKAA 31/03/2017 TSHS. |
|---|---|---|---|---|---|
| | **A: Fedha za Ndani.** | | | | |
| 1 | Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGCDG) | 628,869,599 | 207,050,850 | 22,424,000 | 184,626,850 |
| 2 | Ruzuku ya kujenga Uwezo (CBG) | 69,874,400 | 20,265,000 | 17,815,200 | 2,449,800 |
| 3 | Mfuko wa Jimbo - CDCF (Mchinga) | 35,245,000 | 30,793,902 | 30,793,902 | - |
| 4 | Mfuko wa Jimbo - CDCF (Mtama) | 43,024,000 | 39,505,033 | 33,000,000 | 6,505,033 |
| 5 | Mfuko wa Barabara (Roads Fund) | 745,351,310 | 170,889,897 | 51,247,400 | 119,642,497 |
| 6 | Programu ya Upatikanaji wa Maji Vijijini (RWSSP) | 1,814,950,000 | 352,863,809 | 287,840,400 | 65,023,409 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Shule Maalum (Nyangao) | 100,000,000 | - | - | - |
| 8 | TPDC | 20,000,000 | 20,000,000 | 12,448,400 | 7,551,600 |
| | **Jumla ndogo** | **3,457,314,309** | **841,368,491** | **455,569,302** | **385,799,189** |
| | **B: Fedha za nje.** | | | | |
| 1 | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEDP) | 392,556,000 | - | - | - |
| 2 | Mpango wa Kuinua Ubora wa Elimu Tanzania (EQUIP TZ) | 853,715,000 | 429,782,548 | - | 429,782,548 |
| 3 | Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF) | 532,184,000 | 270,841,911 | 225,498,296 | 45,343,615 |
| 4 | Udhibiti maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto (EGPAF) | 379,739,060 | 8,584,172 | 8,329,250 | 254,922 |
| 5 | Madini Joto (UNICEF) | 45,010,000 | 22,224,500 | 22,224,500 | - |
| 6 | NTDs | 94,000,000 | - | - | - |
| 7 | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(TASAF II) | 5,753,051,496 | 1,548,274,200 | 1,548,274,200 | - |
| | **Jumla ndogo** | **8,050,255,556** | **2,279,707,331** | **1,804,326,246** | **475,381,085** |
| | C: Mchango wa Halmashauri | | | | |
| 1 | Mchango wa Halmashauri | 1,005,422,000 | 424,528,100 | 147,348,737 | 277,179,363 |
| | Jumla ndogo | 1,005,422,000 | 424,528,100 | 147,348,737 | 277,179,363 |
| | **JUMLA - BAJETI YA MWAKA 2016/2017** | **12,512,991,865** | **3,545,603,922** | **2,407,244,285** | **1,138,359,637** |
| | D: Bakaa ya mwaka 2015/2016 | | | | |
| 1 | Mchango wa Halmashauri | 89,632,374 | 89,632,374 | 82,931,300 | 6,701,074 |
| 2 | Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (RWSDP) | 6,773,416 | 6,773,416 | 6,773,416 | - |
| 3 | Mfuko wa Barabara (Road Fund) | 614,728,936 | 614,728,936 | 429,545,665 | 185,183,271 |
| 4 | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEDP) | 540,000,000 | 540,000,000 | 539,431,977 | 568,023 |
| 5 | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(TASAF II) | 25,117,079 | 25,117,079 | 25,117,079 | - |
| 6 | Mpango wa Kuinua Ubora wa Elimu Tanzania (EQUIP TZ) | 658,299,378 | 658,299,378 | 654,753,378 | 3,546,000 |
| 7 | Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF) | 69,100,866 | 69,100,866 | 63,948,297 | 5,152,569 |
| 8 | Mpango wa Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) | 37,646,810 | 37,646,810 | 37,646,810 | - |
| 9 | Kudhibiti maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (EGPAF) | 9,838,102 | 9,838,102 | 9,838,102 | - |
| 10 | Mfuko wa Umwagiliaji wa Wilaya (DIDF) | 214,500,000 | 214,500,000 | 208,617,968 | 5,882,032 |
| 11 | Mfuko wa Jimbo - CDCF (Mchinga) | 2,200,000 | 2,200,000 | 2,200,000 | - |
| 12 | Mfuko wa Jimbo – CDCF (Mtama) | 2,506,082 | 2,506,082 | 2,506,082 | - |
| | **JUMLA BAKAA** | **2,270,343,043** | **2,270,343,043** | **2,063,310,074** | **207,032,969** |
| | **JUMLA KUU TSHS.** | **14,783,334,908** | **5,815,946,965** | **4,470,554,359** | **1,345,392,606** |

Pamoja na jedwali tajwa hapo juu wajumbe walipewa kabrasha lilioonyesha hali halisi ya matumizi ya fedha kwa miradi iliyotekelezwa. Taarifa ilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano.

Katika kujadili taarifa hiyo, kuhusu mbegu za ufuta ambazo zilipelekwa huko vijijini na kuuzwa kwa bei ya Tshs.8000 kwa kilo, wajumbe walipenda kujua baada ya kuuzwa mbegu ya ufuta Halmashauri ilipata faida au hasara.

Katika kujibu hoja hizo Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa lengo hasa la Halmashauri kuhusu mbegu ya ufuta lilikuwa ni kutoa huduma na sio biashara, kwa sasa mbegu zilizobaki zimehifadhiwa kwenye ofisi za Kata.

Aidha, kuhusu mradi wa upimaji wa maeneo ya fukwe wajumbe walisisitiza kuwa, jitihada zifanyike ili maeneo hayo yaanze kupimwa. Katika kujibu hoja hiyo Afisa Ardhi alieleza kuwa tatizo kubwa la kuchelewa kupima eneo hilo hakuna tangazo lililotolewa na Serikali (GN). Kutokana na majibu hayo kikao,

***Ilishauriwa kuwa***, kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira isimamie na ifuatilie upimaji wa fukwe.

Pia, wajumbe walitaka wapewe ufafanuzi kwa nini fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi kutoka ofisi kuu ya Halmashauri kwenda vijijini zinachelewa kupekekwa. Katika kujibu hoja hiyo Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa, fedha zinacheleweshwa kutokana na vijiji husika kukosa akaunti zilizo hai.

Kuhusu mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mwalimu katika shule ya msingi Mtumbya ambayo wananchi walikuwa wanajitolea na walifikia hatua ya msingi, lakini yalitolewa maelekezo na wataalam wa ujenzi kwamba msingi wa nyumba hiyo ubomolewe kwa sababu ulijengwa chini ya kiwango, hatua hiyo, ililalamikiwa na wananchi. Wajumbe walitaka ofisi itoe maelezo ni namna gani itasaidia ujenzi wa nyumba hiyo.

Katika kujibu hoja hiyo Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa atatembelea Mtumbya ili kwenda kuona hali halisi.
Aidha, kuhusu mradi wa upanuzi wa kituo cha Afya Kitomanga kukifanya kiwe Hospitali kwa vile, yametolewa maelekezo na Wizara ya Afya kuwa vituo vya afya visibadilishwe kuwa Hospitali isipokuwa, Halmashauri itenge eneo la kuanzisha Hospitali ya Wilaya. Kutokana na maelekezo hayo,

***ILISHAURIWA kuwa***, Mkurugenzi Mtendaji (W) na wataalam wajenge hoja Wizara ya Afya kwamba Halmashauri iruhusiwe kukifanya kituo cha Afya Kitomanga kuwa Hospitali kwa sababu kazi ya kukibadilisha imefanyika na ipo katika hatua za mwisho na tamko la kukifanya kiwe hospitali lilitolewa na Rais wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete.

Pia,Kamati ya Elimu, Afya na Maji kupitia vikao ifuatilie suala hilo ili kupata mrejesho.

**KUMB. NA. 39/2016/2017 – TAARIFA YA MIHTASARI YA VIKAO VYA KAMATI ZA KUDUMU.**
Taarifa ya mihtasari ya vikao vya kamati za kudumu vilivyofanyika katika robo ya tatu mwezi Januari - Machi, 2017 iliwasilishwa.

Taarifa hizo zilihusisha mihtasari ifuatayo:

- Mihtasari ya taarifa ya vikao vya Kamati ya Fedha , Utawala na Mipango vya tarehe 15/01/2017, 17/01/2017(maalum), 27/02/2017 na 29/03/2017
- Mihtasari ya taarifa ya vikao vya Kamati ya Elimu, Afya na Maji tarehe 11/01/2017 na 13/01/2017(maalum)
- Mihtasari ya taarifa ya vikao vya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira tarehe 09/01/2017 na 11/01/2017( maalum)
- Mihtasari ya taarifa ya vikao vya Kamati ya kudhibiti UKIMWI tarehe 09/01/2017 na 09/01/2017 (maalum)

Taarifa ya Mihtasari ya vikao vya kamati za kudumu ilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano. Katika kupitia na kujadili taarifa za mihtasari hasa za vikao vya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango wajumbe ilishauri na kusisitiza kwamba ofisi iendelee kuomba vibali vya kuajiri watumishi katika maeneo yote yenye upungufu kama vile, Watendaji wa Vijiji na Maafisa Ugani. Baada ya majadiliano ya kutosha,

**ILIAZIMIWA kuwa**, taarifa ya mihtasari ya vikao vya kamati za kudumu, Kamati ya Fedha , Utawala na Mipango vya tarehe 15/01/2017, 17/01/2017(maalum), 27/02/2017 na 29/03/2017, mihtasari ya Vikao vya Kamati ya Elimu, Afya na Maji tarehe 11/01/2017 na 13/01/2017(maalum) , mihtasari ya vikao vya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira tarehe 09/01/2017 na 11/01/2017(Maalum), muhtasari wa kikao cha Kamati ya kudhibiti UKIMWI tarehe 09/01/2017 na 09/01/2017 (Maalum) ilikubaliwa na kupitishwa.

**KUMB. NA. 40/2016/2017 – MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KUDUMU ZA UENDESHAJI MIKUTANO.**

Taarifa ya marekebisho ya kanuni za kudumu za uendeshaji wa mikutano ya Halmashauri za mwaka 2015 iliwasilishwa. Taarifa ya mapendekezo ilieleza kwamba kanuni zilizofanyiwa marekebisho ni kanuni ya 2, kanuni ya 16, kanuni ya 67, kanuni ya 69 na kanuni ya 75.

**Jedwali lifuatalo linaonyesha mapendekezo ya marekebisho ya kanuni**

| NA | KANUNI YA AWALI INAYOTUMIKA | MAREKEBISHO YA KANUNI |
|---|---|---|
| 1 | Marekebisho kanuni ya 2 – kauli zenye kashfa,maagizo ni kwamba kwenye kanuni itajwe tafsiri ya neno kauli yenye kashfa. | Kauli yenye kashfa ni ile inayotolewa kwa maneno au maandishi ikiwa na lengo la kumdhalilisha, kumuumiza na kushusha hadhi ya mtu mbele ya mtu. |
| 2 | Kanuni namba 16 – taratibu za majadiliano kanuni hii ilikuwa inampa maamuzi ya mwisho Mwenyekiti bila kumpa haki mjumbe asiyeridhika na maamuzi ya Mwenyekiti, ilishauriwa kuongeza kifungu kitakacho mpa haki mjumbe asiporidhika. | Pale ambapo mjumbe katika mkutano hatoridhika na maamuzi ya Mwenyekiti atapeleka malalamiko yake kwa Katibu (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri) na Katibu atawasilisha malalamiko kwenye Kamati ya Maadili kwa ajili ya majadiliano na maamuzi. |
| 3 | Kanuni namba 76 – uvunjaji wa mikataba kanuni hiyo imetakiwa iongezwe utaratibu wa uvunjani wa mikataba kwa mujibu wa sheria ya mikataba sura Na. 345 toleo la mwaka 2002 | Pale ambapo mkataba ulitiwa lakiri/muhuri na Halmashauri haukufuatwa na Mkandarasi ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa kimsingi Mkurugenzi Mtendaji (W) atashauriana mapema iwezekanavyo na Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kwa kuzingatia taratibu za mikataba, itaamua hatua muafaka za kuchukua na kumfahamisha mkandarasi juu ya uamuzi. |
| 4 | Kanuni namba 69 – Diwani au Afisa kutokuwa na maslahi kwenye mikataba.kanuni hii imetakiwa iongezwe kanuni ndogo itakayoonyesha kosa na adhabu kwa Diwani au Afisa. | Diwani au Afisa yoyote wa Halmashauri atakaye kiuka vipengele vya kanuni hizo atakuwa ametenda kosa chini ya kifungu cha 120(4) cha sheria ya Serikali za Mitaa kwenye(Mamlaka za Wilaya) sura 287 toleo la 2002, na anaweza kuchukuliwa hatua kwa mujibu kifungu cha 96 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura 16 toleo 2002 |
| 5 | Kanuni namba 75 – ukaguzi wa nyaraka. Kanuni hiyo inampa na vilevile inamnyima haki mjumbe kukagua nyaraka mbalimbali, hivyo imeagizwa kwamba katika kanuni hiyo, kanuni ndogo ya kwanza (75 (1) neno na kama nakala zitapatikana iondolewe. | Hivyo, kanuni hiyo itasomeka mjumbe ataweza, kwa madhumuni ya kutekeleza wajibu wake kama mjumbe, na si vinginevyo, kukagua waraka wowote ambao umejadiliwa na Kamati za kudumu za Halmashauri, anaweza kupewa, akiomba nakala kwa madhumuni hayo hayo |

Mapendekezo ya marekebisho ya kanuni yalipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano.

Katika kujadili mapendekezo hayo wajumbe kwa pamoja walikubali na kupitisha. Kwa hali hiyo,

**ILIAZIMIWA Kuwa,** Mapendekezo ya marekebisho ya kanuni za kudumu za uendeshaji wa mikutano ya Halmashauri, kanuni ya 2,16, 67,69 na 75 yamekubaliwa na kupitishwa.

**KUMB. NA. 41/2016/2017 - MAELEKEZO YA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKATABA NA ZABUNI KWA SERIKALI ZA MITAA**

Maelekezo ya utoaji na usimamizi wa mikataba na Zabuni kwa Serikali za Mitaa yaliwasilishwa. Barua ya maelekezo ya utoaji na usimamizi wa mikataba na zabuni yenye Kumb Na. CAD.35/215/01/53 ya tarehe 10/03/2017 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais ilisomwa kwenye kikao. Kikao kwa kauli moja kilipokea maelekezo na kuzingatia

**KUMB. NA. 42/2016/2017 – KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalam kwa majadiliano mazuri. Aliwaombwa wataalam wafanye kazi kwa bidii kwani Halmashauri haiko vizuri sana kimapato kwa sasa. Aidha, waliombwa Wahe. Madiwani watakapo rudi kwenye maeneo yao wakawahamasishe wananchi palizi la mikorosho wasaidie kudhibiti mianya ya utoroshaji wa mazao mfano, zao la ufuta. Aliwatakia safari njema na alifunga kikao saa 9.00 alasiri.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **SAMWEL W. GUNZAR** | **MATHEI B. MAKWINYA** |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE**......11/08/2017.